

Taarifa ya COVID-19 kwa Wafanyakazi

Kampuni/Kituo [Company/Facility]: _____

Idadi ya matukio katika kiwanda hiki [# cases at this plant]: _____

Tarehe ya taarifa hii [Date of this update]: _____

Jina la kituo cha afya kilicho karibu kinachofanya uchunguzi [Local health center]: _____

Nambari ya simu ya kituo cha afya [Tele# of health center]: _____

COVID-19 inaathiri jumuiya nyingi katika eneo la North Carolina, katika taifa na duniani kote. Hivi karibuni kumekuwa na matukio yaliyothibitishwa miongoni mwa wafanyakazi hapa katika kituo hiki. Tunajali sana afya yako. Tumefanya mabadiliko katika shughuli na sera zetu ili kupunguza hatari ya wewe kupata virusi ili kusaidia kudumisha afya na usalama wako.

Kituo chetu kinashirikiana na maafisa wa afya wa eneo na jimbo ili kusaidia katika kushughulikia matukio haya kwa haraka ili kupunguza kusambaa kwa virusi. Huenda idara ya afya au kituo cha afya kinafuatilia wafanyakazi wenzako, familia na marafiki ambao wamekaribiana na wafanyakazi ambao wamepatikana na virusi ili kubaini iwapo wanaonyesha dalili. Mtu yeyote aliye na dalili anaweza kuelekezwa ili afanyiwe uchunguzi.

Kituo cha afya kilichoorodheshwa hapo juu kinatoa uchunguzi na utathmini wa kimatibabu kufanyiwa uchunguzi kwa mfanyakazi yeyote aliye na dalili za COVID-19 kama vile **kuumwa na kichwa, koo linalowasha, uchovu, kikohozi au homa**. Mtu yeyote aliye na **dalili hatari zaidi kama vile matatizo ya kupumua au kutoweza kutembea bila kusaidiwa** atachunguzwa mara moja na mfanyakazi wa matibabu au kupelekwa kwenye idara ya kushughulikia dharura.

Tunakuhimiza upige simu kazini iwapo wewe ni mgonjwa na ukae nyumbani iwapo unahisi dalili za COVID-19, hata kama una dalili ndogo. Ni muhimu sana kwa mtu yeyote anayehisi dalili za COVID-19, hata dalili ndogo kama vile kuumwa na kichwa na koo linalowasha, kupiga simu kwa kituo cha afya kilicho hapo juu au daktari wako kwa uchunguzi wa kimatibabu na utathmini wa kufanyiwa uchunguzi. Kuchukua hatua hii kutasaidia kudhibiti kiwango cha kusambaa kwa virusi kazini kwako na pia kutasaidia kudhibiti kiwango cha kusambaa kwa virusi katika jumuiya yako. Kwa kuchukua hatua wakati una dalili, unaweza kusaidia kukomesha kusambaa kwa virusi kwa familia na jumuiya yako. Huenda pia ukawa unaokoa maisha ya mtu mwingine ambaye anaweza kuwa katika hatari kubwa zaidi ya kuathiriwa kukuliko, kama vile mzee au mtu aliye na ugonjwa sugu.

Huenda wafanyakazi ambao ni wagonjwa wataombwa kuenda nyumbani au huenda hawataruhusiwa kuingia katika kituo au kuruhusiwa kusafiri kuelekea kwenye kituo. Wafanyakazi walio na dalili na hasa wale wanaopatikana na COVID-19 watahimizwa kujitenga wenyewe kutoka kwa watu wengine wanapoendelea kupata nafuu kutokana na virusi ili wasisambaze virusi kwa wanafamilia, wafanyakazi wenzao au watu wengine.

Iwapo una wasiwasi kuhusu kukosa kuenda kazini, tafadhali wasiliana na msimamizi wako kuhusu sera zetu au kupata usaidizi wowote ambao huenda unastahiki kupata (k.m. ruhusa ya ugonjwa). Wasiliana na kampuni ya bima yako ya afya, kwa kuwa baadhi yazo hazitozi gharama za kuchunguzwa au kutibiwa kwa COVID-19. Iwapo huna bima ya afya, wasiliana na kituo cha afya kilichoorodheshwa hapo juu.

Njia ambazo unaweza kujilinda dhidi ya virusi:

- Kaa umbali wa angalau futi 6 kutoka kwa watu wengine.
- Osha mikono yako vizuri (angalau sekunde 20 kwa kutumia maji na sabuni).
- Usiguse uso wako kwa mikono ambayo haijaoshwa.
- Kohoa au upige chafya kwenye kiwiko cha mkono wako au karatasi ya shashi badala ya mikono yako ili ujilinde na uwalinde watu wengine dhidi ya kupata vijidudu vya maradhi. Usitumie karatasi ya shashi zaidi ya mara moja.
- Tumia barakoa za uso au kitambaa kufunika pua na mdomo wako unapokuwa karibu na watu wengine

